# TANPAWA

Toleo namba 37 | Jarida la Mtandaoni | Septemba 24, 2025

## ZIARA YA MKURUGENZI MTENDAJI WA TANESCO
# BW. LAZARO TWANGE
## KATIKA MIKOA YA KUSINI





TANESCO kuimarisha hali ya upatikanaji umeme kusini



Aridhishwa na maendeleo ya Mradi wa TAZA

JARIDA LA

# TANPAWA




**TANPAWA** – Jarida la TANESCO lenye habari kuhusu maendeleo ya Sekta ndogo ya umeme nchini.

Soma, fahamu, na ungana nasi katika safari ya kuhakikisha umeme wa uhakika kwa Watanzania wote!

Pata Taarifa mbalimbali za **TANESCO** kupitia Whatsap Channel TANESCO YETU kwa Kuscan **QR CODE**

# BODI YA WAHARIRI


| | | |
|---|---|---|
| 01. | **Lazaro J. Twange** | - Mwenyekiti |
| 02. | **Irene Gowelle** | - Mhariri Mkuu |
| 03. | **Augustino Kasale** | - Mhariri |
| 04. | **Amanda Tagame** | - Mwandishi |
| 05. | **Josephine Maxime** | - Mwandishi |
| 06. | **Charles Kombe** | - Mpiga Picha |
| 07. | **Michael Sokotta** | - Msanifu Kurasa |




# YALIYOMO NDANI YA **JARIDA**











**Uk 5.** MD Twange awahakikishia wananchi wa mikoa ya Kusini umeme wa uhakika

**Uk 9.** Maendeleo ya utekelezaji Mradi wa TAZA yanaridhisha - MD Twange

**Uk 12.** MD Twange awapongeza Wafanyakazi, ataka kasi zaidi ya uunganishaji wa umeme

**Uk 14.** RC Mtaka aifagilia TANESCO kwa kuelimisha matumizi ya nishati ya umeme kupikia



# MD TWANGE AWAHAKIKISHIA WANANCHI WA MIKOA YA KUSINI UMEME WA UHAKIKA

- Ni baada ya kusafirishwa kwa Mtambo wa kuzalisha umeme kwa gesi asilia wa **megawati 20**
- Atoa rai kwa watendaji wa TANESCO kupambana na wizi wa umeme na uharibifu wa miundombinu

**Na Josephine Maxime,** Lindi

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO Bw. Lazaro Twange amewaondoa hofu wananchi wa Mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara kuwa Mikoa hiyo itaendelea kuimarika kwa kupata umeme wa uhakika baada ya kuongeza Mtambo wa kuzalisha gesi asilia wa Megawati 20 unaotarajia kuwasili Mkoani Mtwara hivi karibuni.

Hayo aliyasema Septemba 15, 2025 alipofanya ziara katika Mikoa ya Kusini ambapo akiwa katika Mkoa wa TANESCO wa Pwani Kusini eneo la Mkuranga Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa licha ya mchango mkubwa unaofanywa na wafanyakazi amewataka kuongeza kasi ya kupambana na matukio ya wizi wa umeme ambayo yamekuwa yakiripotiwa.





Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO **Bw. Lazaro Twange** akizungumza na baadhi ya wateja wakubwa katika Wilaya ya Rufiji katika ziara yake aliyoifanya ya kukagua maendeleo ya miradi ya umeme katika mikoa ya kusini

*"Endeleeni kupambana na wezi wa umeme ninyi mnahangaika na kazi ya kuwafikishia umeme lakini wapo watu ambao wanafanya vitendo vya wizi kwa lengo la kulipa kiasi kidogo tofauti na matumizi ili TANESCO isipate mapato yake kihalali,"alieleza Bw. Twange.*

Katika hatua nyingine alimtembelea Mkuu wa Mkoa wa Lindi Mhe. Zainabu Telack na kumhakikishia kuwa licha ya Mtambo wa kuzalisha umeme wa Megawati 20 ,TANESCO inafanya jitihada za makusudi za kuendelea kuboresha njia za kusafirisha umeme katika Mkoa huo.

*''Tunafahamu changamoto zilizopo tutahakikisha kwa kutumia miundombinu iliyopo tutaimarisha hali ya upatikanaji umeme kwa Mkoa wa Lindi, tunao mpango mkakati ambao unaonesha jitihada zinazoendelea kufanyika na hivi karibuni tutaanza kuona matokeo,'' alifafanua Bw. Twange.*



Mkurugenzi Mtendaji ametumia sehemu ya ziara yake kutoa majiko yanayotumia umeme kidogo kwa baadhi ya Viongozi wa Serikali akiwemo Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Katibu Tawala wa Mkoa wa Lindi pamoja na Katibu Tawala wa Wilaya ya Rufiji kwa lengo la kuendelea kuhamasisha wananchi juu ya matumizi ya umeme kupikia ambayo ni nafuu na ni rafiki wa mazingira.




# PIKA KWA UMEME NI NAFUU SALAMA NA SAFI KWA MAZINGIRA

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO **Bw. Lazaro Twange** akimkabidhi jiko linalotumia umeme kidogo Mkuu wa Mkoa wa **Lindi** Mhe. Zainabu Telack ili kuendelea kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa kutumia umeme kupikia kwakua ni nafuu ikilinganisha na nishati zingine ikiwa ni kuunga mkono ajenda ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya matumizi ya Nishati Safi ya kupikia.

**Lindi**
**15** SEPTEMBA, **2025**

www.tanesco.co.tz

**#TupoKazini**




# PIKA KWA UMEME NI NAFUU SALAMA NA SAFI KWA MAZINGIRA

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO **Bw. Lazaro Twange** akitoa zawadi ya jiko linalotumia umeme kidogo kwa Mkuu wa Wilaya ya Lindi **Mhe. Victoria Mwanziva** katika Ziara ya Mkurugenzi huyo mikoa ya kusini ya kukagua miradi mbalimbali ya umeme pamoja na kuzungumza na wafanyakazi wa Shirika.

**Lindi**
**15** SEPTEMBA, **2025**



# MD TWANGE ARIDHISHWA NA MAENDELEO YA MRADI WA TAZA – AAGIZA KUONGEZWA KWA KASI YA UTEKELEZAJI

- Asema njia ya kusafirisha umeme wa Msongo wa Kilovoti 400 (203 km) Tunduma – Sumbawanga umefikia zaidi ya **asilimia 79.07**
- Amshukuru **Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuwekeza kwenye miradi ya umeme

Na **Josephine Maxime,** Songwe

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Bw. Lazaro Twange, ameridhishwa na maendeleo ya utekelezaji wa Mradi wa Tanzania-Zambia Transmission Interconnector (TAZA), kupitia njia ya kusafirisha umeme wa Msongo wa kilovoti 400 (203 Km) Tunduma Sumbawanga ambao kwa sasa umefikia zaidi ya asilimia 79.

Alisema Mradi huo unalenga kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika katika mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe na Rukwa, na hivyo kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa maeneo hayo.

Katika ziara yake Mkoani Songwe na Mbeya Septemba 18, 2025 Bw. Twange alisisitiza umuhimu wa wakandarasi kuongeza kasi ya kazi ili kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati, kama ilivyopangwa katika mikataba.

> "Kwanza tunamshukuru **Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kutupa fedha za kutekeleza miradi, kazi hii sio ndogo lakini maendeleo ni mazuri, kwa mfano katika njia ya kusafirisha umeme wa Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Tunduma hadi Sumbawanga, mkandarasi amesema tayari amesimamisha nguzo 171 kati ya 497 kazi yetu ni kumsimamia amalize kwa wakati ," alisema Bw. Twange.

Katika kituo cha kupoza Umeme cha Malangali, ambacho ni miongoni mwa vituo vitano vinavyotekelezwa chini ya mradi wa TAZA, Bw. Twange alieleza kuwa maendeleo yamefikia asilimia 36. Amemtaka Mhandisi anayesimamia Mradi huo kuongeza usimamizi wa karibu kwa mkandarasi.

Bw. Twange ametumia nafasi hiyo kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uwekezaji mkubwa katika sekta ya umeme, akisisitiza kuwa hatua hii inaonesha dhamira ya dhati ya Serikali katika kukuza uchumi wa nchi kupitia Sekta ya umeme.

Mbali na mradi wa njia ya kusafirisha umeme Tunduma–Sumbawanga, Mkurugenzi Mtendaji pia alitembelea Kituo cha kupoza umeme cha Iganjo kilichopo Mkoani Mbeya, pamoja na Kituo cha Nkangamo kilichopo Tunduma, mkoani Songwe, ambapo amewahakikishia wananchi kuwa TANESCO iko imara katika kutekeleza miradi na kuwahudumia wananchi.

Hii ni ziara maalumu aliyoifanya katika mikoa ya Kusini ambapo licha ya kukutana na wafanyakazi wa mikoa hiyo, ametembelea vituo vya kuzalisha Umeme kwa gesi asilia Mtwara 1 na 2, pamoja na Miradi mbalimbali ikiwemo Kituo cha kupoza Umeme Songea – Tunduru, Kituo cha kupoza Umeme Mradi wa TAZA Malangali – Sumbawanga, Kituo cha kupoza umeme Nkangamo Tunduma – Songwe, Kituo cha kupoza umeme Iganjo Mbeya pamoja na njia ya kusafirisha umeme Msongo wa Kilovoti 400 (203 Km) Tunduma – Sumbawanga.





# MATUKIO KATIKA PICHA

MD TWANGE ARIDHISHWA NA MAENDELEO YA MRADI WA **TAZA**










# MD TWANGE APONGEZA WAFANYAKAZI, ATAKA KASI ZAIDI YA UUNGANISHAJI UMEME KATIKA MIKOA YA KUSINI

- Asisitiza Mpango wa Misheni 300 ni agizo la **Mhe. Rais Dkt Samia Suluhu Hassan**
- Ataka kuongeza wigo wa kuwasiliana na wateja katika mikoa mbalimbali.

Na **Josephine Maxime,** Rukwa

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Bw. Lazaro Twange, amewapongeza wafanyakazi wa TANESCO kwa jitihada zao katika kutoa huduma bora kwa wateja, huku akiwataka kuongeza kasi katika utekelezaji wa Mpango wa Misheni 300, unaolenga kuongeza idadi ya wateja wanaounganishiwa umeme nchini.

Akiwa Mkoani Njombe, Septemba 17, 2025 Bw. Twange alisisitiza kuwa utekelezaji wa mpango huo ni agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, hivyo lazima utekelezwe kwa mafanikio ya asilimia 100.

> “Malengo mliojiwekea ya asilimia 80 hayatoshi, tunahitaji kuona asilimia 100 ya uunganishaji wa wateja. Haya ni maagizo ya Mheshimiwa Rais, na maagizo yake hayawezi kujadiliwa bali kutekelezwa kwa vitendo,” alisisitiza Bw. Twange.

Katika kuimarisha huduma kwa wateja, Bw. Twange aliwataka maafisa uhusiano na huduma kwa wateja kuongeza idadi ya wateja wanaowasiliana nao, kuhakikisha taarifa muhimu za Shirika zinawafikia angalau kwa asilimia 50 ya wateja wote katika kila Mkoa.



Katika ziara yake Mkoani Rukwa, Bw. Twange alipongeza kasi nzuri ya ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wateja, alisisitiza kuwa mapato hayo ndiyo yanayotumika kuendesha shughuli za Shirika na kuchochea maendeleo ya wafanyakazi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala, Bi. Margareth Mwandu, aliwataka wafanyakazi kuongeza ubunifu na uwajibikaji, alibainisha kuwa changamoto nyingi za msingi tayari zimetatuliwa na sasa ni wakati wa kuonesha matokeo.

Ziara yaBw. Twange ililenga kukagua maendeleo ya miradi ya umeme, kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa umeme kwa viongozi wa Serikali pamoja na kuzungumza na Wafanyakazi wa Mikoa ya Kusini.

# MATUKIO KATIKA PICHA

**MD TWANGE** AKIZUNGUMZA NA WAFANYAKAZI KATIKA MIKOA YA KUSINI









# ZIARA YA MD TWANGE YAENDELEA MIKOA YA KUSINI

- Aifikia mikoa ya Ruvuma na Mtwara
- Akagua miradi mbalimbali ya umeme Pamoja na kuifikisha elimu ya nishati safi ya kupikia kwa umeme

Na **Josephine Maxime**

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO Bw. Lazaro Twange ameendelea na Ziara yake katika mikoa ya Kusini wa Tanzania ambapo amekagua miradi mbalimbali ya umeme, kutoa elimu ya nishati safi ya kupikia kwa umeme Pamoja na kuzungumza na wafanyakazi ili kuboresha ufanisi wa kuwahudumia watanzania.

Akiwa Mkoani Ruvuma Bw. Twange alikagua maendeleo ya Kituo cha kupoza umeme cha Songea – Tunduru ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 50.6 ya utekelezaji wake ambao utakapokamilika utachangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme mikoa yote ya Kusini.

Aidha, alitembelea Ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo Mhe. Brigedia Jenerali Ahmed Abas Ahmed ambapo miongoni mwa mengi waliyozungumza alielezea juu ya namna TANESCO imejipanga kuimarisha umeme katika Mkoa wake, Mkurugenzi Mtendaji alimkabidhi jiko la umeme linalotumia umeme kidogo ikiwa ni jitihada za kuendeleza kutoa elimu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Hata hivyo katika Mkoa wa Mtwara alizitambua changamoto mbalimbali za umeme Mkoani humo Pamoja na kueleza namna zinakwenda kutatuliwa kutokana na miradi ya umeme inayoendelea.

Alifanya pia mazungumzo na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe. Kanali Partick Sawala ambapo alimhakikishia kuwa TANESCO imejipanga kuimarisha hali ya umeme katika Mkoa wake ikizingatiwa imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kutatua changamoto za umeme Mkoani humo.

Huu ni mwendelezo wa Ziara za Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO mikoa ya Kusini ,ambazo zimeleta matokeo makubwa kwa wafanyakazi wa TANESCO katika utendaji kazi ambapo mazingira yao ya kazi yameimarishwa kwa kiasi kikubwa huku changamoto zao zikitatuliwa lakini pia utambuzi wa changamoto mbalimbali zinazofanya ukosefu wa umeme mikoani humo na mwarobaini wa tatizo hilo.




# PIKA KWA UMEME NI NAFUU SALAMA NA SAFI KWA MAZINGIRA

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO **Bw. Lazaro Twange** akimkabidhi jiko linalotumia umeme kidogo Mkuu wa Mkoa wa **Mtwara, Mhe. Kanali Patrick Sawala** ikiwa ni sehemu ya jitihada za TANESCO za kuendelea kuhamasisha matumizi ya umeme kupikia kwa kuwa ni salama, nafuu na rafiki kwa mazingira.

**Mtwara**
**16** SEPTEMBA, **2025**




# PIKA KWA UMEME NI NAFUU SALAMA NA SAFI KWA MAZINGIRA


Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma **Mhe. Brigedia Jenerali Ahmed Abasi Ahmed** akikabidhiwa jiko linalotumia meme kidogo na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO **Bw. Lazaro Twange** ili kuwa balozi wa elimu ya umuhimu wa kutumia nishati ya umeme kupikia kwa wananchi kwa kuwa ni nafuu zaidi kulinganisha na nishati zingine.

**Ruvuma**
**16** SEPTEMBA, **2025**

# MATUKIO KATIKA PICHA

MKURUGENZI MTENDAJI WA TANESCO **BW. LAZARO TWANGE** NA MKUU WA MKOA WA NJOMBE **MHE. ANTONY MTAKA** WAKIWA KATIKA PICHA YA PAMOJA NA BAADHI YA WAFANYAKAZI WA TANESCO MAKAO MAKUU NA WAFANYAKAZI KUTOKA OFISI YA MKUU WA MKOA WA NJOMBE





Pata **Taarifa** na **Huduma** Mbalimbali Kupitia **Mitandao** Yetu ya **Kijamii**




@tanesco_official_page

@tanescoyetu

@tanescoyetutz

www.tanesco.co.tz

0758 346 869



Limetolewa na:
Kurugenzi ya Mawasiliano na Huduma kwa Wateja,
**TANESCO** Makao Makuu, Dodoma.

---

**TANESCO YETU**
WhatsApp Channel

**FOLLOW US**

www.tanesco.co.tz